# KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO

# KONFERENSI YA KASKAZINI MASHARIKI MWA TANZANIA

## SEMINA ELEKEZI
## KWA MAKARANI WA MAKANISA

# "NAMNA YA KUANDIKA MINITI ZA KIKAO"

CONFIDENTIAL

**IMEANDALIWA NA KUSANYWA**

**NA**

**MCHUNGAJI MUSA E. NZUMBI**

**KATIBU MKUU NETC**

**2017**

# KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO – SAME
# S.L.P 315, SAME
# KIKAO CHA BARAZA LA KANISA
# KILICHOFANYIKA KANISA LA SDA SAME MJINI
# TAREHE 22 DESEMBA 2015

**AGENDA**:

1. Tamko la Utume
2. Kaulimbiu ya "Utume Kwanza"
3. Mkutano Mkubwa ya Injili.
4. Mwinjilisti Mlei Eneo jipya
5. Ununuzi wa Kiwanja – Kirinjiko
6. Uhamisho wa Washiriki Wanaotoka
7. Uhamisho wa Washiriki Wanaoingia
8. Ujenzi wa kanisa
9. Msisitizo wa Uwakili
10. Kuunda kamati ya Manunuzi
11. Kuunda kamati ya Majengo
12. Mkataba wa Mlinzi wa Kanisa
13. Nidhamu ya Kanisa.
14. Bajeti ya Kanisa Mwaka 2016
15. Kupitisha Majina ya Waalimu wa Shule ya Sabato.
16. Kupitisha Majina ya Waimbaji wa Kwaya ya Kanisa

CONFIDENTIAL

| | | |
|---|---|---|
| PR NIKOMBOLWE KIRAVU | MWENYEKITI | WAJUMBE WALIOHUDHURIA |
| SIFAEL MBONEA | KATIBU | |

SAMWELI ANDREA, SILAS ELIRAHA, RUTH MJEMA, ISSAH YOHANA, DANIEL MARTIN, MUKAMA SOSPETER, REHEMA JOSEPH, ZAKAYO MFINANGA, ROSEMARY BENARD, MAGRETH TIMOTHEO, JONATHANI IBRAHIMU, EMMANUEL BARNABA, JEREMIAH MKAZENI.

| | |
|---|---|
| 1. MIKA ROBERT<br>2. NANZIA STANLEY<br>3. PETRO DANIEL<br>4. SELEMANI ABBAS | WAJUMBE WASIOFIKA KWA TAARIFA |

| | |
|---|---|
| 1. HULDA JOHNSON<br>2. ESTHER ZAWADI<br>3. BETHSHEBA MISANA<br>4. HERBERT KIGORA<br>5. DAWSON GODFREY<br>6. FARAJA LUSIU | WAJUMBE WASIOFIKA BILA TAARIFA |

| | |
|---|---|
| 1. MR ADILI NDIMANGWA (Mchungaji Mwanafunzi UoA)<br>2. ENG JOHN PAUL (Injinia Mshauri katika Agenda ya Ujenzi) | WAJUMBE WAALIKWA |

| | | |
|---|---|---|
| NZK NO: 59 | Fanyeni Kazi Zenu, Usiku si mbali. | WIMBO WA KUFUNGUA |
| Ndg Jeremiah Mkazeni | | OMBI LA KWANZA |
| Mch Nikombolwe P. Kiravu. | Yohana 3:16 Kazi kubwa ya Kanisa ni Kuutangaza Upendo mkuu wa Mungu kwa kumtoa Yesu Kristo, hivyo tuna wajibu wa kuhakikisha kila mtu anaandaliwa kuokolewa na kuupata uzima wa milele. | NENO LA UFUNGUZI |

CONFIDENTIAL

Ndg Emmanuel Barnaba na Mrs Rosemary Benard

MAOMBI BAADA YA NENO

PENDEKEZO: Kusomwa Tamko la Utume la Kanisa la WaAdventista wa Sabato

TAMKO LA UTUME
**001**

PENDEKEZO: Kuikubali Kaulimbiu ya Kanisa Ulimwenguni inayosema "UTUME KWANZA NI WAKATI WA MAVUNO" na kusisitiza kaulimbiu hiyo kupitia njia zifuatazo hapa kanisani:

1. Kutengeneza mabango ya utume
2. Kwaya kutunga nyimbo za utume,
3. Kila mshiriki kuwa na roho 2 kwa mwaka.

KAULIMBIU YA UTUME KWANZA
**002**

KWA KUWA: Kanisa letu limemaliza mwaka mzima wa 2014 bila kuwa na mikutano ya hadhara, na kwa kuwa aina ya uinjilisti inayofaa kwa sasa kulingana na mazingira ya hapa wilayani ni Mikutano Mikubwa ya Hadhara,

PENDEKEZO: Kuwa na Mkutano mkubwa wa injili hapa Wilayani Same.

i. Tarehe 1-21 April 2016.
ii. Mahali: Ni Viwanja vya Stand Kuu.
iii. Mhubiri: Mchungaji Abby Katete kutoka Mtaa wa Mbauda.
iv. Kwaya: Kurasini SDA Choir kutoka Dar es Salaam.
v. Idara ya Huduma iandae mapendekezo ya kamati za Efoti hii na kuleta mapendekezo kikao kijacho cha baraza.
vi. Timu ya wainjilisti walei iandaliwe na kuingia nyumba kwa nyumba kuandaa efoti hiyo.

MKUTANO MKUBWA WA INJILI
**003**

CONFIDENTIAL

KWA KUWA: Mgagao ni moja ya Maeneo Mapya na yenye Changamoto kubwa ya Malezi hasa kwa kuwa ni eneo la Umasaini ambapo linahitaji Mwinjilisti Mlei wa karibu, na kwa kuwa Familia ya Mr Jonathan Mdee wamekuwa tayari kutoa nusu ya gharama za kumlipa posho Mwinjilisti, na kwa kuwa tayari Kamati ndogo ya Uinjilisti chini ya Mkuu wa Idara ya Huduma wameleta pendekezo la Mwinjilist Gerald Ole Sembeho kuwa Mwinjilisti eneo hilo jipya, na kwa kuwa Ole Sembeho yuko tayari kutumika na utaratibu ulishafuatwa kupitia Kanisa lake na Mchungaji wake,

PENDEKEZO: Kupitisha Jina la Mwj Gerald Ole Sembeho kuwa mwinjilist wa kanisa letu eneo la Mgagao kama ifuatavyo:

1. Utaratibu wa wito wake uzingatiwe ikiwa ni pamoja na bima na barua iandikwe kwenda conference.
2. Idara ya Amo ikabidhiwe jukumu la kuandaa vyombo vya kuanzia maisha.
3. Kanisa litamchukua kwa miezi 3 ya majaribio kuanzia Januari 1, 2015 ndipo afanye kwa mwaka mzima kuanzia Marchi 1, 2015 hadi Marchi 30, 2015.
4. Mkataba wa maandishi ujazwe kati yake na kanisa, ili kuliweka kanisa salama.
5. Pawe na tathmini ya maendeleo ya kazi yake itakayoletwa na kujadiliwa na baraza la kanisa.
6. Kanisa lipange kumpatia Pikipiki ya Kumwezesha kufanya kazi kwa kasi na ufanisi mkubwa – idara ya huduma iratibu jambo hilo.

MWJ OLE SEMBEHO KUWA MWINJILISTI ENEO JIPYA –MGAGAO

**004**

CONFIDENTIAL

KWA KUWA: Kijiji cha kirinjiko ni moja ya maeneo mapya katika kanisa letu, na kwa kuwa mikutano mingi ya efoti imefanyika na watu wengi kubatizwa, na kwa kuwa waumini hawa hawana eneo la kuabudia.

PENDEKEZO: Kuidhinisha shilingi 500,000 kutoka kwenye bajeti ya kanisa ili isaidie ununuzi wa Kiwanja cha kujengea kanisa

500,000TSH KWA UNUNUZI WA KIWANJA KIRINJIKO

005

PENDEKEZO: Uhamisho wa Washiriki Kutoka Kanisa Letu na Kwenda Makanisa Mengine Kama ifuatavyo:

1. Ndg James Ibrahimu – Kwenda Kanisa la SDA Manzese- Dar Es Salaam
2. Mrs Pendo Gilbert – Kwenda Kanisa la SDA Longido.
3. Ndg Joakimu Lugwisha – Kwenda Kanisa la Kamunyonge – Musoma.
4. Ndg Herbert Kilongora – Kwenda Kanisa la SDA Texas - Marekani

UHAMISHO WA WASHIRIKI WANAOTOKA
**006**

PENDEKEZO: Uhamisho wa Washiriki Kutoka Makanisa Mengine Kuja Kanisa Letu Kama ifuatavyo:

1. Ndg Pius Labani kutoka Kanisa la Kibamba SDA – Dar.
2. Ndg Togolani Eliamani Kutoka Kanisa la Mbeya Kati SDA – Mbeya
3. Mrs Haika Pendaeli Kutoka Kanisa la Majengo SDA – Moshi.
4. Ndg Yohana Andrea Kutoka Kanisa la Kwakilacha- Suji

UHAMISHO WA WASHIRIKI WANAOINGIA
**07**

KWA KUWA: Jengo la Kanisa tulilopo sasa limekuwa dogo, na limechakaa, na kwa kuwa idadi ya waumini imeongezeka na kiwanja tulicho nacho ni kikubwa kujenga kanisa linguine, na kwa kuwa hata idara ya majengo imeshaanza mchakato wa namna ya kuanza mipango hii:

PENDEKEZO: Kukubali wazo la Kuanza rasmi ujenzi wa Jengo la Ibada kama ifuatavyo.

1. Vipimo vya ujenzi viwe (MT 60 kwa 40)
2. Idara ya Majengo iandae gharama za ujenzi (BOQ kuanzia Msingi hadi kumalizia).
3. Idara ya Majengo ifatilie Kuomba kibali cha Ujenzi kutoka ofisi za Ardhi Wilaya, kabla ya February 7, 2015.

UJENZI WA JENGO LA KANISA
**008**

CONFIDENTIAL

4. Idara ya Majengo iandae ratiba ya Changizo kubwa  mwezi Marchi litakalokuwa na lengo la kukusanya Milion40 ya kuanzia ujenzi.
5. Ratiba za Kuombea ujenzi huu ifanyike kila sabato ili Mungu aongoze mwenyewe.

PENDEKEZO: Kulikubali wazo la Msisitizo wa Uwakili kwa kila mshiriki kama lilivyoletwa na NETCO na kulisisitiza wazo hili kanisani kwetu kupitia program zifuatazo:

1. Kila mwanakikosi wa Shule ya Sabato
2. Kila mwanafunzi wa darasa la Ubatizo,
3. Kamati ya Uwakili ya Kanisa
4. Somo la Uwakili wakati wa Efoti za Hadhara,
5. Kutengeneza masanduku ya sadaka,

MSISITIZO WA UWAKILI **009**

CONFIDENTIAL

PENDEKEZO: Kuunda kamati ndogo ya Utaratibu wa Manunuzi ya Kanisa

1. Ndg Joseph Masalu – Mwenyekiti
2. Ndg Mashauri Yonaza- Mjumbe
3. Mrs Rose Mukama- Mjumbe
4. Dr Yohana Mkwizu – Mejumbe
5. Ndg Helington Magessa – Mjumbe

Hadidu za Rejea:

- ✓ Kamati hii itakutana kila mara wakati wa manunuzi.
- ✓ Kamati italeta mapendekezo yake kwenye Baraza la Kanisa.
- ✓ Kamati inapaswa kukusanya angalau quortation tatu.

KAMATI YA MANUNUZI YA KANISA **010**

PENDEKEZO: Kuunda Kamati ya Majengo ya Kanisa kama ifuatavyo:

1. Mzee Zephania Maganga – Mwenyekiti
2. Eng Patroba Kimbute – Katibu Mr
3. Ndg Yohana Mdee – Mjumbe
4. Mrs Penina Mkazeni - Mjumbe
5. Mama Eunice Msemo – Mjumbe

Hadidu za Rejea

KAMATI YA MAJENGO **011**

- ✓ Watakutana kila robo mara moja
- ✓ Wataangalia mahitaji ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya kanisa,
- ✓ Watasimamia uchoraji wa ramani ya jengo la kanisa.

KWA KUWA: Mkataba wa Mlinzi anayelinda kanisa unamalizika mwishoni mwa mwezi huu wa Disemba, na kwa kuwa Mlinzi aliyepo ameonyesha kuwa mwaminifu na kufanya kazi yake vizuri,

PENDEKEZO: Kuongeza Mkataba wa Mlinzi wa Kanisa ndugu Jofrey Hosea kwa mwaka mmoja kwa mapendekezo yafuatayo.

1) Mlinzi atajaza Mkataba na Kutia saini yake.
2) Kumuongezea Posho yake kutoka 80,000 hadi 100,000 kwa mwezi,
3) Kumuomba Shemasi Mkuu Kumsimamia mlinzi awe anafika kwa muda na kukabidhi lindo kwa wakati

KUONGEZA MKATABA WA MLINZI
**012**

KWA KUWA: Pamekuwa na muda mrefu wa kushughulikia nidhamu ya Ndugu Domean John kwa sababu ya kuvunja Amri ya Saba, na kwa kuwa idara ya Mashemasi imefatilia jambo hili kwa Umakini Mkubwa ikiwa ni pamoja na kuonana na mhusika naye na kukiri kuvunja amri hiyo, na kwa kuwa kwa muda wa miezi mitatu hii kanisa limekuwa likitafta ukweli wa jambo hili na kujiridhisha kuwa utaratibu umefuatwa hasa wa Mathayo 18:15-17

PENDEKEZO: Kufutwa ushirika wa ndugu Domean John kwa sababu ya kuvunja Amri ya Saba.

KUFUTWA USHIRIKA DOMEAN JOHN
**013**

PENDEKEZO: Kupitisha Mapendekezo ya Bajeti ya Kanisa 2016 kama yalivyoletwa na kamati ya Bajeti **(Angalia Kiambatanisho Na 1)**

BAJETI YA KANISA KWA MWAKA 2016

CONFIDENTIAL

| | | |
|---|---|---|
| PENDEKEZO: | Kupitisha Mapendekezo ya Waalimu na Viongozi wa Vikosi vya Shule ya Sabato kama yalivyoletwa na idara ya shule ya sabato **(Angalia Kiambatanisho Na 2).** Pamoja na marekebisho yafuatayo:<br>1. Semina namna ya kufundisha lesoni iandaliwe na itolewe sabato ya kwanza ya 2015.<br>2. Vikosi hivi vipewe nafasi ya kukutana katikati ya juma.<br>3. Viongozi wa kanisa wapangwe kwenye vikosi kuimarisha uhai wa vikosi.<br>4. Pawe na darasa la waalimu wa Watoto. | WAALIMU WA VIKOSI VYA SHULE YA SABATO<br>**014** |
| PENDEKEZO: | Kupitisha Mapendekezo ya Majina ya Waimbaji wa Kwaya ya Kanisa kama yalivyoletwa , **(Angalia Kiambatanisho Na 3).** Pamoja na Mapendekezo yafuatayo:<br>1. Kila mwanakwaya ajaze fomu ya kujiunga.<br>2. Muda wa mazoezi yao usiingilie shughuli za idara zingine hapa kanisani. | MAJINA YA WAIMBAJI KWAYA YA KANISA 2016<br>**015** |

ZAKAYO MFINANGA — OMBI LA MWISHO

__________________________ __________________________

MCH: NIKOMBOLWE KIRAVU — SIFAEL MBONEA

MWENYEKITI — KATIBU

# MHURI WA KANISA

CONFIDENTIAL

**MAMBO MUHIMU YA KUKUMBUKA:**

I. Namba ya maamuzi ya mwisho itasomeka SAME SDA 015/6/2015 (015 ni namba ya pendekezo, 6 ni ukurasa wa miniti, na 2015 ni mwaka husika kikao kilipofanyika)
II. Baraza linalofuata litaanzia pendekezo namba 016.
III. Kila baraza linapokwisha ni wajibu wa mwenyekiti na katibu wa kikao kutia saini hizo miniti mwishoni na kugonga mhuri wa kanisa mahalia.
IV. Mfumo huu wa uandishi unatumika kwa mabaraza yote: mabaraza ya kanisa, mabaraza ya mtaa, Halimashauri ya Kanisa, mabaraza ya wazee, mabaraza ya kanda, mabaraza ya idara nk…
V. Viambatanisho vyote vya kufafanua agenda kwa kuwa maranyingi huwa ni maelezo marefu au vithibitisho zaidi ya page moja huambatanishwa nyuma ya miniti, hii ni pamoja na orodha ya waimbaji wa kupitisha, bajeti ya mwaka, nk…

CONFIDENTIAL

**KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO - SAME**
**KIKAO CHA BARAZA LA KANISA**
**KILICHOFANYIKA KANISA LA SDA SAME MJINI**
**TAREHE 22 DESEMBA 2015**

**KIAMBATANISHO CHA ORODHA YA MAHUDHURIO**

| NA | JINA LA MJUMBE | NAFASI YA MJUMBE | SAHIHI YA MJUMBE |
|---|---|---|---|
| 01 | MCH NIKOMBOLWE P. KIRAVU | MWENYEKITI | |
| 02 | SIFAEL MBONEA | KATIBU | |
| 03 | SAMWELI ANDREA | MJUMBE | |
| 04 | SILAS ELIRAHA | MJUMBE | |
| 05 | RUTH MJEMA | MJUMBE | |
| 06 | ISSAH YOHANA | MJUMBE | |
| 07 | DANIEL MARTIN | MJUMBE | |
| 08 | MUKAMA SOSPETER | MJUMBE | |
| 09 | REHEMA JOSEPH | MJUMBE | |
| 10 | ZAKAYO MFINANGA | MJUMBE | |
| 11 | ROSEMARY BENARD | MJUMBE | |
| 12 | MAGRETH TIMOTHEO | MJUMBE | |
| 13 | JONATHANI IBRAHIMU | MJUMBE | |
| 14 | EMMANUEL BARNABA | MJUMBE | |
| 15 | JEREMIAH MKAZENI | MJUMBE | |
| 16 | | | |
| 17 | | | |
| 18 | | | |
| 19 | | | |
| 20 | | | |
| 21 | | | |
| 22 | | | |
| 23 | | | |
| 24 | | | |
| 25 | | | |
| 26 | | | |
| 27 | | | |
| 28 | | | |
| 29 | | | |
| 30 | | | |

CONFIDENTIAL

## Kiambatanisho No 1
## Orodha ya Majina ya Waimbaji wa Kwaya ya Kanisa

1 Rosemary Benard
2 Magreth Timotheo
3 Jonathan Ibrahimu
4 Maige Jeremiah
5 Igubilo Makindigi
6 Joseph Msemakweli
7 Lydia Lupilya
8 Imakulata Hosea
9 Julius Idrisa Joseph
10 Jane Imram
11 Kurwa Imanuel
12 Elizabeth Joshua
13 Alphonce Perege
14 Lois John
15 Ivanaice Charles
16 Godfrey Mathias
17 Yona Gaga
18 Hellen Mpumilwa
19 Sarah Silas
20 Rebeca Praygord
21 Julieth Justine
22 Jonas Gombelesa
23 Cathbert Jonathan
24 Dorah Mtaita
25 Ntegenjwa Tarusi
26 Ibrahim Thomas
27 Yohana Mariko

CONFIDENTIAL

***Mwisho wa Semina***